

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/58

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA

3 Barabara ya Rashidi

Kawawa,

S.L.P 5429,

12880 -DAR ES SALAAM.

Tanzania

17/05/2019

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

MKOA WA DAR ES SALAAM WAZIDI KUJIIMARISHA KATIKA MAKUSANYO YA KODI.

Katibu tawala wa Mkoa wa Dar es salaam Bw. Abubakar Kunenge amesema Mkoa huo umeendelea kuweka mipango madhubuti ya kuhakikisha unaendelea kuongoza kitaifa katika suala zima la ukusanyaji wa mapato pasipo kuwabugudhi wananchi kwa kubuni vyanzo vipya vya mapato.

Akizungumza wakati wa kikao cha kutoa maoni ya mikakati ya kuboresha mapato ya Serikali katika mkoa wa Dar Es Salaam ulioshirikisha wadau mbalimbali ikiwemo Watafiti, Wataalamu na Taasisi mbalimbali, Bw. Kunenge amesema mkoa huo una kila sababu ya kuwa kinara wa ukusanyaji mapato hivyo Serikali ya mkoa itahakikisha wanaendelea kuwa kinara.

Aidha Bw.Kunenge amesema ndani ya Mkoa huo wapo wataalamu, watafiti, vyyuo na makampuni ya ushauri ambayo mawazo yao yakitumika vizuri yataweza kusaidia kuongoza mapato.

"Tumeona tunaweza kufanya vizuri hivyo tumetumia nafasi hii kuomba makampuni, wataalamu, walimu wafanya biashara na wadau mabalimbali watakao tusaikia kutushauri katika suala zima la ukusanyaji wa mapato na kutoa maoni yao kutusaikia jinsi ya tuboresha kupata mapato ya Mkoa wa Dar Es Salaam ilikumsaidia Mh Rais Katika kukamiliaha miradi ya maendeleo" alisema Bw.Kunenge

Kwa upande wake Katibu mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara Bw. Joseph Simbakaria alisema anatoa pongezi kwa wafanya kazi wa Mkoa wa Dar es salaam wakiongozwa na Mhe.Paul Makonda kwa kufanya kazi nzuri ya ukusanyaji wa Mapato, na kuona umuhimu wa kukaa na wadau wa biashara kuangalia jinsi gani wanaweza kusaidia mapato ya Mji Mkuu wa Biashara Dar es Salaam" alisema Bw.Joseph.

"Napenda kutoa pongezi kwa wafanya kazi wa mkoa wa Dar es salaam wakiongozwa na Mhe. Paul Makonda kwa kufanya kazi nzuri ya ukusanyaji wa Mapato, na kuona umuhimu wa kukaa na wadau wa biashara kuangalia jinsi gani wanaweza kusaidia kuongeza mapato ya Mji Mkuu wa Biashara japo Mji Mkuu ni Dodoma ila kibiashara ni Dar es salaam" alisema Bw.Joseph.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM